



TAARIFA KWA UMMA

Dodoma 10 Julai, 2026

Wizara ya Afya inasikitika kutoa taarifa kwa wadau wa afya na umma kwa ujumla kuwa kuna kikundi cha matapeli kinachojitambulisha kwa watu kuwa kina uhusiano wa karibu na Waziri wa Afya, na hivyo kuwarubuni kuwa kinaweza kuwawezesha kukutana na Waziri kwa lengo la kupata ajira na tenda za Serikali.

Kikundi hicho kimekuwa kikitumia mbinu mbalimbali kufanikisha utapeli huo, ikiwemo kuwapigia simu wananchi au kuwasiliana nao ana kwa ana.

Wizara inapenda kutoa ufafanuzi kuwa Waziri wa Afya hajawahi kumtuma, kumuidhinisha wala kumpa mamlaka mtu au kikundi chochote kutoa ahadi ya ajira au tenda za Serikali kwa niaba yake au kwa niaba ya Wizara.

Aidha, Wizara inatoa wito kwa mtu yeyote ambaye amewahi kutapeliwa au kuombwa fedha kwa kisingizio hicho kutoa taarifa haraka kwa vyombo vya dola ili hatua stahiki za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Wizara inasisitiza kuwa mtu yeyote anayehitaji huduma au taarifa kutoka Wizara ya Afya anaweza kufika kupitia taratibu rasmi zilizowekwa na kupata huduma kutoka kwa viongozi na watendaji wa Wizara, akiwemo Katibu Mkuu na maafisa wengine wenye mamlaka. Aidha, Ofisi ya Waziri ipo wazi na inapatikana kupitia taratibu rasmi bila malipo yoyote.

Imetolewa na;

John Mapepele

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

